# Learning by Ear 2012 – Corruption – The Elephant in the Room

## Episode 10 – "Tackling the Elephant"

**Text: Victoria Averill**

**Editing: Johannes Beck, Friederike Müller, Pendo Paul**

**Proofreading: Charlotte Collins, Pendo Paul**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

CHARACTERS:

- NARRATOR

Scene 1:

- Sylvia (FEMALE, 19)
- Isaac (MALE, 22)
- Lydia (FEMALE, 16)
- Crowd (about 5 persons, male and female mixed)

Scene 2:

- Jennifer (FEMALE, 55)
- Alfayo (MALE, 58)
- Jeffrey (MALE, 58)
- Sylvia (FEMALE, 19)

Scene 3:

- TV Anchor/Newsreader (FEMALE, 40)
- Sylvia (FEMALE, 19)
- Jeffrey (MALE, 58)
- Journalist 1 (FEMALE, 30)
- Alfayo (MALE, 58)
- Lydia (FEMALE, 16)
- Isaac (MALE, 22)
- Jennifer (FEMALE, 55)

**Intro:**

**0. Narrator:** Hujambo na karibu kwa sehemu ya kumi na ya mwisho kwenye mfululizo huu wa mchezo wa redio kuhusu ufisadi kwa jina "**Tembo nyumbani**". Katika kipindi kilichotangulia mkereketwa wa kupambana na ufisadi, Jeffrey Thiongo, kwa mara nyingine anakabiliwa na vitisho anapoendelea kufanya kampeni zake za ubunge. Naye Alfayo Odhiambo anatahadharishwa kujiandaa kwa hali yoyote baada ya kufichua kashfa katika sekta ya nishati.

Katika sehemu hii ya mwisho kwa jina "**Kumkabili Tembo**" ni siku ya uchaguzi na sakata linalowahusisha mawaziri serikalini limewekwa wazi kupitia vyombo vya habari. Nini kitakachotomkuta waziri husika na ambaye pia ni mgombea wa urais, John Maina? Na je, Jeffrey atafaulu kuchaguliwa kuingia bungeni? Endelea kusikiliza...

**Scene One:**

**1. Atmo:** **City ambience - Busy street, cars, people talking**

**2. Sylvia:** Pesa chukueni lakini kura msiwapigie! Usidanganyike. Kura kwa Jeffrey Thiongo. Komesha ufisadi- mpe kura yako Jeffrey Thiongo. Usidanganyike, pesa chukueni lakini kura msiwapigie!

**3. Isaac:** Sina hakika kama Jeffrey atafaulu kuingia bungeni. Hebu tazama inavyoonekana watu wengi wanamuunga mkono Jeffrey .

**4. Sylvia:** Tusubiri matokeo Isaac. Kwa muda wa wiki chache zilizopita tumekosa usingizi tukifanya kampeni. Ujumbe

wa Jeffrey ulikuwa mfupi sana na ulio wazi. Nadhani watu watamuunga mkono.

**5. Lydia:** **(shouting)** Isaac, Sylvia, mmesoma gazeti ya leo? Hebu soma!

**5a. SFX:** newspaper noise

**6. Isaac:** Oh Mungu wangu…..ni kuhusu lile sakata la nishati? Na kwanini wamechapisha picha ya babangu sambaba na ya waziri wa nishati, John Maina? Si watu watafikiri pia babangu anahusika katika kashfa hii!

**7. Sylvia:** Lakini Isaac, yeye ni mhusika mkuu, ingawa hakufahamu mapema mtego huu. Kampuni yake ndiyo iliyokuwa ikiuza vifaa na mita za umeme. Na hii, ndiyo sababu aliweza kufichua kashfa hii. Yeye anafahamu yote yaliyokuwa yakiendelea katika sakata hili. Hebu tazama, babangu na waziri Maina, katika ukurasa wa kwanza, ingawa gazeti limeandika wazi kwamba babangu ndiye mwenye kufichua kashfa hii. Aliingizwa bila ya yeye mwenyewe kujua.

**8. Lydia:** Lakini hiyo si kinga, chochote chaweza kutokea. Huwezi kujua madhumuni ya waandishi wa magazeti. Jinsi wanavyokuelezea hutegemea ni nani wanayemuunga mkono kisiasa katika uandishi wao. Na isitoshe wao pia ni binadamu wanaweza kula rushwa. Mimi na Tekla tuna bahati sana majina yetu hayajatajwa mahali popote isipokuwa tu kuandika kuhusu visa vya ulaji rushwa shuleni.

**9. Isaac:** Ni kweli. Maskini babangu! Amechapishwa katika ukurasa wa kwanza katika gazeti la kitaifa, Lydia. Watu wote kote nchini watasoma na kuona picha yake.

**10. Lydia:** Ahhh – Gazeti la leo ndio taka ya kesho. Lakini kusema kweli kitakachowavutia watu wengi zaidi ni huyu waziri wa kazi, John Maina. Hebu tazama, ameangaziwa kama mhusika mkuu katika sakata hili kisha katika siku muhimu kama hii ya uchaguzi! Hii itamharibia sana, sivyo?

**11. SFX:** **Police siren**

**12. Crowd:** **(shouting from far)** Mwizi! mwizi !mwizi!

**13. Sylvia:** Kunaendelea nini ?

**14. Lydia:** Ni maofisa wa usalama! Wamemfunga pingu John Maina! Kisha wanaondoka naye katika gari la polisi!

**15. Isaac:** Lydia, sipendi mazingira ya hapa tena. Mambo yanaweza kuharibika. Hebu tazama tayari raia wameanza kuwakabili maofisa wa usalama. Tuondoke?

**16. Lydia:** Sawa tunaweza kuondoka! Hata hivyo, shughuli ya upigaji kura itamalizika katika muda wa saa moja na nusu hivi. Nafikiri bora tuondoke hapa kabla mambo kuchafuka zaidi.

**17. Isaac:** Twendeni kukutana na mama, baba na Jeffrey. Nadhani hawajapata habari za kukamatwa kwa John Maina?

**End of Scene One**

## Scene Two:

**18. Atmo:** **Restaurant noises, TV on in the background**

**19. Jennifer:** Alfayo, una uhakika tuko salama hapa? Hutaki kwenda nyumbani au katika ofisi za shirika la komesha ufisadi,

**20. Alfayo:** Kwani nini, Jennifer?

**21. Jennifer:** Unajua… Umechapisha katika ukurasa wa kwanza wa gazeti la leo Alfayo. Ni siku ya uchaguzi na ndiyo siku kashfa hii ya kawi imewekwa hadharani. Watu wanaweza kuwa wanakutafuta...Kumbuka Helen kutoka shirika la Jeffrey ametutahadharisha.

**22. Alfayo:** Jennifer, siwezi kurudi nyumbani au kwenda ofisini sasa. Suala hili linanitatiza akili sana, unafahamu vyema kwamba nisingeweza kumfanyia kampeni Jeffrey na badala yake kuwaachia jukumu hilo watoto wetu. Sasa kituo cha kupigia kura kimefungwa, nataka kubaki hapa pamoja na jamaa, mafariki na familia yangu kumuunga mkono Jeffrey hadi matokeo yatakapotolewa, sawa?

…Hata hivyo, Heleni anasema kuwa usalama umeimarishwa baada ya serikali kuongeza idadi ya maofisa hao wa usalama.

**23. Jennifer:** **(sighing)** Ni sawa nilikuwa na wasiwasi tu kuhusu usalama wako... ahhh, Jeffrey amewasili.

**24. Alfayo:** Bw, Thiongo! Habari ya shughuli rafiki yangu? Unajisikiaje sasa?

**25. Jeffrey:** Naendelea vizuri tu, ingawa bado nina wasiwasi sana. Sasa shughuli ya kupiga kura imemalizika na kura zimeanza kuhesabiwa. Lakini sote tunafahamu kwamba visa vya udanganyifu vinaweza kutokea wakati wowote hasa wakati wa kuhesabiwa kura hizo. Chochote chawezekana, kwani ni lini tumeshuhudia matokeo ya ukweli?

**26. Alfayo:** Mmmm… Sijawahi maishani mwangu.

**27. Jeffrey:** Oh Alfayo, nimesahau kukwambia. Nimeona picha yako imechapishwa katika ukurasa wa mbele wa gazeti. Mambo yatalipuka sasa. Unajihisi vipi sasa. Uko sawa?

**28. Alfayo:** Asante sana Jeffrey, najua nimefanya jambo linalostahili. Nina wasi wasi kuhusu yale yatakayotokea baadaye, lakini kufikia sasa macho yote yako kwako zaidi na yule mlaghai Maina wala sio mimi na familia yangu. Naomba hali hii iendelee hivyo.

**29. Sylvia:** **(just arriving out of breath at the restaurant)** Hamjambo.. Samahani kwa kuwakatiza Jeffrey...lakini hebu tazama televisheni! Tazama yanayoendelea!

**30. Jeffrey:** Wanamkamata John Maina! John Maina amewekwa pingu! **(laughs delightedly)** Sikudhani ningeweza kushuhudia kisa kama hiki maishani mwangu!

**End of Scene Two**

**31. Narrator:** Harakati za Jeffrey sasa zimeanza kuzaa matunda. Amefanya juhudi bila kuchoka kupambana na ufisadi, kufikia kiwango cha kupoteza kazi yake. Lakini je, ameweza kuwashawishi wapiga kura? Jibu tutalipa muda si mrefu endelea kusikiliza!

**Scene Three:**

**32. SFX:** **TV-news opener, restaurant ambience in background**

**33. TV Anchor:** Shughuli ya kuhesabu kura sasa imemalizika na kinachosalia ni kusubiri matokeo ya kwanza ya uchaguzi mwa mwaka huu, yanayotarajiwa kutangazwa muda mchache kuanzia sasa.… **(pause)** Naam .. Matokeo ya kwanza yanaonyesha kwamba rais wa sasa amehifadhi kiti chake kuhudumu kwa kipindi kingine. Hatahivyo, lakini chama chake kimepata pigo kubwa. Katika tukio ambalo halikutarajiwa Jeffrey Thiongo na chama chake cha kupambana na ufisadi kimeshinda viti katika sehemu zote za humu nchini! Jeffrey Thiongo pia ameshinda kiti cha ubunge kwa kura nyingi zaidi..**(fade out)...** Hatahivyo, lakini kama tulivyotangulia kusema, haya ni matokeo ya

kwanza tu. Matokeo kamili yatatolewa wiki ijayo. Endelea kuwa nasi kwani muda si mrefu tutawaletea taarifa ya kuhusiana na uchaguzi huu.

**34. Crowd:** **(loud cheers, singing)** Jeffrey! Jeffrey! Jeffrey!

**35. Sylvia:** **(shouting)** Jeffrey, umeshinda!

**36. Jeffrey:** Tumefaulu, Sylvia! Ama kwa hakika nisingeweza kufaulu bila ya usaidizi na juhudi zenu. Nawashukuru sana kwa msaada huo. Asanteni sana! Hapana shaka haya ni matokeo ya kuridhisha. Leo ni siku njema. **(to everybody in the room)** Nawashukuru nyote kwa kuniunga mkono. Na sasa vita dhidi ya ufisadi vimeanza rasmi! Tukomeshe ufisadi sasa!

**37. Crowd:** **(loud cheers, singing)** Jeffrey! Jeffrey! Jeffrey!

**38. Journalist 1:** Bw. Thiongo, mimi ni mwandishi kutoka kituo cha utangazaji cha Capital. Hapana shaka umefurahishwa sana na matokeo haya. Je ni jambo ulilolitarajia?

**39. Jeffrey:** Sikutarajia kabisa, nashangaa kwamba tumeweza kushinda viti vingi kote nchini. Kwa hakika ni matokeo ya kutia moyo sana. Lakini sijashangaa kwamba watu wanakiu cha kumaliza ufisadi humu nchini. Hatimaye, wamepata chama cha kukipigia kura- Chama kinachotetea maslahi yao.

***KW begin***

**40. Journalist 1:** Ni nini utakachokipa kipau mbele pindi utakapofika bungeni?

**41. Jeffrey:** Kitu cha kwanza kabisa, ni kuimarisha juhudi za kupambana na ufisadi shuleni. Tutahakikisha tunapitisha sheria ya kupambana na udanganyifu au matokeo bandia ili watoto wetu wakue wakifahamu kwamba, ufisadi sio maisha.

***KW end***

**42. Journalist 1:** Asante sana Bw. Thiongo. **(to Alfayo)** …Samahani wewe ni Bw. Alfayo Odhiambo, Yule aliyefichua kashfa katika sekta ya nishati?

**43. Alfayo:** Errmm… ndio... ndio, Ni mimi.

**44. Journalist 1:** Huna hofu yoyote kwamba huenda maisha yanaweza kuwa magumu zaidi Bw. Odhiambo? Ninachomaanisha ni ni kwamba baada ya kukamatwa waziri wa nishati, huoni bado kuna watu wanaoweza kukuandama…

**47. Alfayo:** Ndio, nafahamu hilo kwamba bado nimo hatarini. Lakini baada ya kufahamu kilichokuwa kikiendelea, singeweza kukubali kujihusisha na maovu hayo, yaani kujihusisha na visa vya kuwanyang'anya raia wenzangu, ili kuwatajirisha walaghai. Nafahamu nakabiliwa na wakati mgumu sana, lakini nitasimama imara. Natarajia kuwa watu watanielewa. Lakini sasa tuko hapa kusherehekea ushindi wa Jeffrey!

**46. Atmo:** **Crowd celebrating**

**47. Sylvia:** Pongezi! Pongezi! … **(room quietens)** Kwanza kwa babangu kwa ujasiri wake wa kutenda mambo ambayo si wengi wetu wanaweza kuyafanya!

**48. Sylvia/Lydia/Isaac/Jennifer/Jeffrey/Crowd:** Kwa babangu! Alfayo!

**(clinking of glasses)**

**49. Lydia:** Pia ningetaka kumpongeza mama Jennifer. Yeye ametuwezesha kudumisha maadili mema maishani, Ametufunza kwamba maisha si mkato, kwamba tusichukue hongo na badala yake kupambana na ufisadi.

***KW begin***

**50. Isaac:** Ni kweli, Lydia - pongezi kwa mama kwa kutuelekeza njia ifaayo. Ni vigumu sana kudumisha maadili mema maishani katika mazingira yaliyozungukwa na ufisadi huku kukiwa hakuna hata mtu mmoja wa kukemea uovu huo. Isitoshe ni mtu anayesimamia ukweli na kupinga ufisadi. Haogopi kupambana na tembo nyumbani.

***KW end***

**50. Sylvia/Lydia/Isaac/Alfayo/Jeffrey/Crowd:** Kwa mama Jennifer. Jennifer! **(clinking of glasses)**

**51. Jennifer:** Asanteni sana. Ni kweli Isaac si rahisi. Lakini Jeffrey na chama chake pamoja na shirika la kukomesha ufisadi sasa amesaidia sana kutuonyesha barabara nzuri. Sasa tunafungua ukurasa mpya wa maisha bila ufisadi na

uchaguzi huu umetuonyesha kwamba watu wanatuunga mkono!

**52. Everyone:** Kwa Jeffrey! Kwa shirika la Kukomesha Ufisadi Sasa! Kwa maisha yetu ya baadaye bila ufisadi! **(cheers)**

**End of Scene Three**

**MUSIC (FADE UNDER OUTRO)**

**53. Narrator:** Na hadi hapo tunafika mwisho wa mchezo huu wa redio kuhusu Ufisadi kwa jina "**Tembo Nyumbani**" Hadithi inayoelezea maisha halisi ambayo imeandikwa na Victoria Averill.

Endapo unataka kusikiliza kipindi hiki au vingine katika mfululizo wa mchezo huu, tembelea mtandao wetu wa dw.de/lbe

Na pia unaweza kutuandikia, kutueleza maoni yako kuhusiana na vita hivi dhidi ya ufisadi. Pia unaweza kuungana nasi kupitia ukurasa wetu wa Facebook. Hadi wakati mwengine, kwaheri na asante kwa kutusikiliza!